


# Kipimo cha Ngozi cha TB (Mantoux)

Kipimo cha ngozi cha Kifua kikuu (TB), wakati mwengine huitwa “Mantoux,” ni namna rahisi, isiyokuwa na madhara ya kujua kama una maambukizo ya TB iliyolala.



## Ni nini maambukizo ya TB iliyolala?


Kuna hatua mbili za TB. Hatua zote mbili zinaweza kutibiwa na dawa. Viini vya TB vinapoingia mwili wako kwa mara ya kwanza, vinasababisha maambukizo ya TB iliyolala. Bila matibabu, maambukizo ya TB iliyolala yanaweza kuwa ugonjwa wa TB unaoweza kusababisha madhara. Mtu yeyote anaweza kupata TB kwa sababu inaenea kutoka kwa mtu mmoja hadi mwengine kupitia hewa.

Hatua ya 1 – Maambukizo ya TB Iliyolala	Hatua ya 2 – Ugonjwa wa TB Inayosababisha Madhara
Viini vya TB vime“lala” ndani ya mwili wako. Hatua hii inaweza kudumu mda mrefu sana – hata miaka mingi.	Viini vya TB viko madhubuti na vinaenea. Zinaharibu tishu za mwilini mwako.
Hauonekani mgonjwa wala haujisikii mgonjwa. X-rey yako ya kifua kawaida huwa iko imara.	Kawaida huwa unajisikia mgonjwa. Daktari wako atafanya vipimo maalum atambue ni wapi mwili wako unadhurika na TB.
Hauwezi kueneza TB kwa watu wengine.	Kama viini vya TB viko ndani ya mapafu yako, unaweza kueneza TB kwa watu wengine kwa kukohoa, kuchemua, kuongea, au kuimba.
Kwa kawaida inauguliwa kwa kutumia dawa moja kwa miezi 9.	Inatibiwa kwa kutumia dawa 3 au 4 kwa angalau miezi 6.

## Nitajuaje kama nina maambukizo ya TB iliyolala?

Kipimo cha ngozi cha TB (“Mantoux”) kinaweza kuonyesha kama una maambukizo ya TB iliyolala. Unaweza kuwa na maambukizo ya TB iliyolala ikiwa umewahi kukaribiana na mtu mwenye ugonjwa wa TB unaoweza kusababisha madhara (hata kama haukujua ni wagonjwa).

Mhudumu wako wa afya atatumia sindano ndogo na aweke majimaji fulani yasiokuwa na madhara (yanaitwa “tuberculin”) kwa ndani ya ngozi ya mkono wako.



Mhudumu wako wa afya **LAZIMA** akague mkono wako siku 2 au 3 baada ya kipimo cha ngozi cha TB, hata kama wewe unaona mkono wako unaonekana sawa.

## Nitashughulikia vipi mkono wangu baada ya kipimo cha ngozi cha TB?

- Usizibe pahali na bandeji au tepu.
- Fanya makini usifikiche wala usikune.
- Mahali pakikuwasha, weka kitambaa cha baridi jua yake.
- Unaweza kuosha mkono wako na kuukausha kwa makini.



## **Kipimo cha Ngogzi cha TB (Mantoux) – ukurasa wa 2**

**Usiogope kupimwa.  
TB inaweza kutibika!**

### **Je kama kipimo changu cha ngozi cha TB sio hakika?**

Kipimo ni “sio hakika” kama hakuna uvimbe (au kuna uvimbe mdogo sana) mahali ambapo majimaji yaliwekwa. Kipimo cha ngozi cha TB ambacho sio hakika kawaida humaanisha kuwa hauna TB.

Katika baadhi ya hali, huenda utahutaji kipimo cha ngozi cha TB chengine tena baadaye.

### **Je kama kipimo changu cha ngozi cha TB ni hakika?**

Kipimo ni “hakika” ikiwa kuna uvimbe wa kiasi fulani mahali ambapo majimaji yaliwekwa. Inamaanisha huenda una viini vya TB katika mwili wako. Watu wengi wenye kipimo cha ngozi cha TB hakika wana maambukizo ya TB iliyolala. Ili uwe na hakika, daktari wako atakugua na akufanyie x-ray ya kifua. Huenda utahitaji vipimo vyengine ujue kama una ugonjwa TB inayosababisha madhara.

**Dumisha afya yako na ya jamii yako —  
kapate kipimo cha ngozi cha TB!**

Ili uweze kupata kipimo cha ngozi cha TB, wasiliana na daktari wako au na idara yako ya afya ya jamii.

### **Unapswa kufanyiwa kipimo cha ngozi cha TB kama:**

- umekaribiana mara kwa mara na mtu mwenye ugonjwa wa TB inayosababisha madhara,
- kama ume ishi katika nchi ambapo watu wengi wana TB,
- unafanya kazi na au unaishi katika nyumba ya mauguzi (nursing home), kliniki, hospitali, jela, au hifadhi ya watu wasiokuwa na makaazi (homeless shelter), au
- umeambukizwa HIV au matatizo mengine ya afya.

### **Je kama nimeshapata chanjo ya BCG?**

Hata kama umepata chanjo ya BCG, pia unaweza kupata kipimo cha ngozi cha TB.

- Watu ambao wameshapata chanjo ya BCG pia wanaweza kuwa na maambukizo ya TB iliyolala na ugonjwa wa TB inayosababisha madhara.
- Chanjo ya BCG inaweza kukusaidia kuwakinga watoto wadogo wasiugue sana na TB. Kinga hufifia jinsi watu wanavyoendelea kukuwa na kuzeeka.
- Chanjo ya BCG wakati mwengine husababisha ishara za kipimo cha ngozi cha TB hakika. Lakini ukiwa na ishara hakika kwa kipimo cha ngozi cha TB, labda yatokana na virusi vya TB katika mwili wako – sio kutokana na chanjo yako ya BCG.

**Unaweza kupata kipimo cha ngozi cha TB, hata kama umeshapata chanjo ya BCG!**

**Oregon**  
**Health**  
Authority  
PUBLIC HEALTH DIVISION  
HIV, STD and TB Section